جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات

# Je, uliwahi kujiuliza: Ni nani aliyekuumba? Na ni kwa nini? Na ni nini kitakuwa baada ya kifo?

هَلْ سَأَلْتَ نَفْسَكَ؟ مَنْ خَلَقَكَ؟ وَلِمَاذَا؟ وَمَاذَا بَعْدَ المَوْتِ؟

Kiswahili

سواحيلي

Kamati ya Kisayansi ya Jumuia ya Huduma ya Maudhui za Kiislamu kwa Lugha mbalimbali

# هَلْ سَأَلْتَ نَفْسَكَ؟ مَنْ خَلَقَكَ؟ وَلِمَاذَا؟ وَمَاذَا بَعْدَ المَوْتِ؟

## **Je, uliwahi kujiuliza: Ni nani aliyekuumba? Na ni kwa nini? Na ni nini kitakuwa baada ya kifo?**


اللَّجْنَةُ العِلْمِيَّةُ
بِجَمْعِيَّةِ خِدْمَةِ المُحْتَوَى الإِسْلَامِيِّ بِاللُّغَاتِ

Kamati ya Kisayansi ya Jumuia ya Huduma ya Maudhui za Kiislamu kwa Lugha mbalimbali

بِسْمِ اللهِ الرَّحمَنِ الرَّحِيمِ

## Je, uliwahi kujiuliza: Ni nani aliyekuumba? Na ni kwa nini? Na ni nini kitakuwa baada ya kifo?

Ni nani aliyekuumba ewe mwanadamu? Lau ungelitazama kiwiliwili chako kwa kutumia darubini, basi ungeona ulimwengu mwingine kabisa wenye ufanisi mkubwa na ushindi. Kwani, kila seli ndani ya mwili wako inabeba taarifa za kijeni zenye misimbo tata. Je, uliwahi kujiuliza ni nani aliyeumba misimbo hii? Na ni nani aliyeiweka katika sehemu yake sahihi?

Kila jengo madhubuti, na kila nyumba iliyotulizana, inaelezea kisa cha mtengenezaji wake. Hivi je, inaingia akilini kutokea kwa ulimwengu huu mpana pamoja na uzuri wake na ufanisi wake na mpangilio mzuri wa vipengele vyake pasina mtengenezaji?!

Ewe mwanadamu, kama ambavyo akili yako haikubali kuambiwa kwamba kuna simu mahiri iliyotengenezwa kwa ufanisi wa hali ya juu ambayo ilitokeza ghafla bila ya kuwepo wa

kuibuni na kuitengeneza, au kwamba kuna mtandao mgumu sana wenye vifaa vya vinavyofanya kazi kwa uzuri na ufanisi mkubwa bila ya kuwepo yeyote aliyeuunda wala kuusimamia. Hivyo hivyo, akili haikubali kuambiwa kwamba ulimwengu huu mkubwa pamoja na kila kilichomo miongoni mwa mipangilio madhubuti, ubunifu na kanuni zenye ufanisi mkubwa ulipatikana bila muumbaji?!

Bila shaka kila kipande katika ulimwengu huu, kuanzia punje ndogo kabisa mpaka kundi kubwa zaidi la nyota ni ishara inayoonyesha utukufu na ukubwa wa muumbaji wake. Haiingii akilini kwamba mfumo huu nyeti ulianza kwa fujo tu. Bila shaka akili inakataa kuwa ulimwengu huu ulianza bila ya muumbaji au kwamba mfumo huu tata na wa hali ya juu ni matokea ya tukio la ghafla lilitokea kipofu!

Na kama ambavyo akili sahihi na maumbile yaliyo sawa vinamuongoza mwanadamu katika kuamini uwepo wa muumbaji wa ulimwengu, basi vile vile mambo hayo mawili yanatuongoza kuzingatia sifa za Muumbaji huyu na haki zake

juu yetu.

Hakika kuzitafakari sifa za Muumbaji huyu kunatufungulia sisi milango ya ufahamu wa kina kuhusu ulazima wa kusifika kwake na sifa za ukamilifu mkubwa zaidi na kutasika kwake mbali na kila mapungufu.

Hayo yanamaanisha kuwa Muumbaji huyu anasifika na kila sifa za uzuri na utukufu. Kwani Yeye aliyetakasika ndiye muweza mno wa kila kitu, Mwenye kujua kila kitu, Mwenye hekima katika kila alichokiumba na kupanga. Ukamilifu huu si tu kwamba ni kitu kinawezakuwa, bali ni jambo la lazima kiakili. Kwa sababu kuwepo mapungufu yoyote katika sifa zake ni kutalazimu kuwepo mapungufu katika uumbaji na upangiliaji, jambo ambalo linapingana na uhalilisia tunaouona katika ufanisi wa hali ya juu wa ulimwengu huu.

Kama ambavyo kumtakasa kutokana na mapungufu kunalazimu kwamba Muumbaji huyu ni mwenye kujitosheleza na hawahitaji viumbe wake, bali hata hahitaji yeyote. Bali wote ni wahitaji kwake katika uwepo wao na

kusalia kwao. Naye Mtukufu ametakasika kutokana na mshirika na mtoto, kwa sababu hayo ni katika alama za mapungufu na kushindwa, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametakasika kutokana na hayo yote.

Akiwa Mwenyezi Mungu ndiye muumbaji Mtukufu mwenye kusifika kwa sifa za ukamilifu na utukufu, na Yeye ndiye aliyetufanya kuwepo na akaufanya ulimwengu kuwepo baada ya kutokuwepo, na Yeye ndiye Mmilika wa yote yaliyo ndani yake, na Yeye ndiye anayeturuzuku na kutuzingira kwa rehema yake, na Yeye ndiye mpangiliaji mwenye mwenye kuendesha kila kitu; hivi si wajibu kwetu kumshukuru na tutafute ni namna gani tutapata radhi zake na jinsi gani tutatekeleza haki yake ya wajibu juu yetu na tufanye ili kutimiza lengo alilotuumba kwa ajili yake?!

Je ni mantiki kuwa Mwenyezi Mungu atuumbe kisha asituwekee wazi ni kipi anachokitaka kutoka kwetu? Kwa nini sisi tuko hapa? Ni lipi lengo na dhumuni la uwepo wetu katika maisha? Nini kitatutokea baada ya kufa?

Tafakari pamoja nami lau kama mtu atajenga kasri la kifahari, na akaweka humo vifaa vya kiteknolojia vya kisasi, mpaka akawa ameshakamilisha kuliimarisha na kuliboresha, kisha ghafla akaanza kulibomoa lote kwa ujumla pasina sababu. Je, inawezekana kumsifia mtu huyu kuwa ana busara? Je, si jambo la kawaida kabisa kukichukulia kitendo hiki kuwa ni upuuzi usioendana na mtu mwenye akili timamu?

Kwa hivyo, ikiwa kitendo hiki ikiwa hakikubaliki kwa mwanadamu, basi inakuwaje tuwaze kuwa Mwenyezi Mungu Mwenye hekima na Mwenye habari zote kuwa aliumba ulimwengu huu wenye uzuri mkubwa, madhubuti na wenye ufanisi na ufundi wa hali ya juu, kisha aubomoe pasina lengo au hekima yoyote?!

Mwenyezi Mungu wanadamu kwa hekima kubwa, nayo ni kumuabudu Yeye pekee asiye na mshirika. Na aliwaumba ili kuwatahini katika dunia hii, na akawawekea miadi ambayo watafufuliwa ndani yake Siku ya Kiyama ili waulizwe kujukumika juu ya matendo yao. Kwa

hivyo, atakayemuamini Mwenyezi Mungu na akaitikia wito wake, basi atakuwa na neema ya Pepo, adumu humo milele. Na atakayepuuza haki, basi atakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.

Hivyo ibada ni haki ya wajibu juu yetu kwa sababu ndiyo lengo la kuwepo kwetu, na ndio ushahidi wa shukurani yetu na kukiri kwetu kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mola Mlezi na Mungu.

Tafakari kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyekuumba na akakukirimu kwa uwezo wa kusikia na kuona, na akakuzingira kwa neema zisizohesabika. Yeye ndiye anayeipitisha damu katika mishipa yako, na anakuruzuku maji na hewa, na wewe kila wakati unamhitajia. Lau kama si rehema yake na utunzaji wake, basi ungeangamia na zingeteketea nguvu zako. Lakini Yeye Mtukufu alibeba jukumu la kukuruzuku ilhali bado wewe ni kijusi ndani ya tumbo la mama yako, huku hujiwezi na huna uwezo wa kujimilikia chochote.

Hivi muumbaji huyu Mtukufu hastahiki

kuabudiwa kama atakavyo Yeye, si kama utakavyo wewe?! Tafakari lau kama utataka kumpa zawadi mama yako, je kweli ungechagua zawadi inayoridhisha matamanio yako, au ungejitahidi kutaka kujua kila anachokipenda ili umfurahishe kwa kila kinachomfaa? Hivyo hivyo hata kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakufai kuwa kwa mujibu wa matamanio yetu au desturi zetu za kurithiwa. Bali ni kama alivyotaka Yeye Mtukufu, na kwa namna aliyotuamrisha.

Ni lazima ibada iwe halisi na iliyotakasika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee, asiye na mshirika. kwa hivyo, mwanadamu haruhusiwi kufanya ibada kwa ajili ya asiyekuwa Muumba wake. Na dhambi kubwa zaidi linalowajibisha kukaa Motoni milele ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Hilo huwa pindi mwanadamu anamuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu miongoni mwa viumbe vyake, kama vile kuabudu masanamu au jua au mwezi, au kumuabudu mtu au mnyama au mtu mwema. Yote hayo ni miongoni mwa aina za ushirikina na ukafiri, na atakayekufa akiyafanya

hayo, basi malipo yake yatakuwa ni kukaa milele daima katika Moto wa Jahanamu.

Bila shaka Mwenyezi Mungu alituma Manabii na Mitume wengi ili watueleze lengo la kuwepo kwetu duniani na lengo la maisha. Na wajumbe wote ujumbe wao ulikuwa mmoja, ambao ni ujumbe wa Uislamu na kuwaita watu kuja kumuabudu Muumba pekee asiye na mshirika. Lakini wako waliopotosha na kubadili yale waliyokuja nayo Mitume waliotangulia. Basi Mwenyezi Mungu akamtuma wa mwisho wa Mitume, Muhammadi, na akamteremshia ujumbe wa mwisho kwa wanadamu, nao ni Qur'ani tukufu. Kuna ushahidi mwingi sana wa kiakili na wa kisayansi unaothibitisha kuwa Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na kuwa ndicho kitabu cha pekee ambacho hakijawahi kukumbwa na upotoshwaji na ubadilishwaji. Mwenyezi Mungu alitueleza katika Qur'ani kuwa yeye hatokubali kutoka kwa mwanadamu yeyote dini isiyokuwa Uislamu, na kwamba Mitume wote ujumbe wao ulikuwa mmoja: Nao ni kuwaita watu wampwekeshe Muumbaji

na kumuabudu yeye pekee asiye na mshirika. Na akatueleza Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani kuwa kuna Pepo na neema za kudumu watakazopata Waumini, na kuna Moto na adhabu chungu watakayopata wanaoabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu au waliokataa kuingia ndani ya Uislamu.

Kinachoutofautisha Uislamu na dini zingine nikuwa waislamu ndio watu pekee wanaoweza kuleta ushahidi wa kiakili na ugunduzi wa kisayansi, kwa kutegemea vyanzo vya taarifa vya kuaminika, kwa ajili ya kuthibitsha kuwa Qur'ani tukufu iliyoko mikononi mwao ndio maneno ya Mwenyezi Mungu muumba Mtukufu, kilichohifadhiwa kutokana na mabadiliko na upotoshwaji.

Qur'ani tukufu ndicho kitabu ambacho amekiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Nabii wake Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, na amewapa changamoto wanadamu tangu zaidi ya karne kumi na nne walete mfano wake, au hata sura moja mfano wake, wakashindwa hilo, na bado changamoto inaendelea mpaka leo hii pasina yeyote kuweza

kuleta chochote chenye kufanana nayo katika balagha (ufasaha) na ubainifu wake, na utoaji changamoto, na uwekaji sheria, pamoja na hivyo hajaweza yeyote kwa zama na zama kuleta chochote mfano wake, au hata chenye kuikaribia. Ushindi ulioko ndani ya Qur'ani si tu pekee katika lugha yake ambayo imefikia kiwango cha juu cha ufasaha na ubainifu, bali inakwenda mbali ili ukusanye ushahidi wa kiakili na wa kisayansi unaotilia mkazo kuwa kweli ni maneno ya Mwenyezi Mungu. Ikiwa Qur'ani tukufu imekusanya ushahidi wa wazi unaothibitisha kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu, basi maamuzi ya kiakili na ya kimantiki anayofaa mtu kufanya ni kuiamini na kuyafuata yaliyokuja ndani yake, badala ya kutegemea vitabu vingine vilivyoathiriwa na mikono ya watu wakati wa utunzi wake.

Akili salama inatuongoza kuwa maneno ya muumbaji, aliyebuni vizuri ulimwengu na akautengeneza madhubuti mfumo wake, ndio chanzo cha kweli zaidi cha kujua uhakika wa mambo. Na tunapopata ushindi mkubwa ulioko ndani ya Qur'ani katika lugha yake, mambo ya

uhakika wa kisayansi, na utungaji sheria uliokamilika, ongeza pamoja na kuhifadhiwa kwake dhidi ya upotoshwaji kwa zama na zama, hapa hakuna njia ya kukwepa zaidi ya kukubali kuwa haya ni maneno ya Mwenyezi Mungu.

Pamoja na hivyo, kuamini yote yaliyokuja ndani ya Qur'ani si tu jambo la hiyari ya kiimani, bali ndio maamuzi ya kiakili yanayoendana na mantiki ya kutafuta uhakika.

Na alibainisha Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur'ani tukufu kuwa hakutuumba bure kwa mchezo, bali alituumba kwa ajili ya kumuabudu.

Na alitueleza Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani kuwa maisha haya ya Dunia tunayoishi ni hatua tu ya muda mfupi na itamalizika hivi karibuni, lakini maisha ya kweli na ya milele yatakuwa Akhera pale watakapoingia Waumini Peponi na Makafiri Motoni.

Muumbaji aliyetuleta kutoka katika kutokuwepo, ana uwezo kwa msisitizo mkubwa kabisa wa kuturejesha katika maisha baada ya kifo. Kwani katika yale yanayotuzunguka

miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, tunashuhudia ushahidi wa kihisia juu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu usioisha katika kuhuisha yaliyokufa. Kwa hivyo, kama ambavyo Mwenyezi Mungu hutoa moto katika mti mbichi, na akatoa mazao na matunda kutoka katika Ardhi kavu, na akaumba kijusi ndani ya tumbo la uzazi la mama yake kutokana na tone la manii, basi yeye Mtukufu ni muweza wa kuhuisha wafu na kuwafufua kutoka makaburini mwao kwa ajili ya malipo Siku ya Kiyama. Kwani, Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu. Na miongoni mwa uonevu na dhuluma ni kumalizika kwa maisha ya aliyedhulumu na aliyedhulumiwa pasina kuulizwa juu ya matendo au kulipwa.

Na anaweza kujiuliza mwanadamu kwa nini Uislamu tu na isiwe dini nyingine isiyokuwa Uislamu?

Bila shaka kikubwa kinachomtofautisha mwanadamu na viumbe wengine ni akili, na kazi yake kubwa ni kutafakari na kutafuta uhakika wa mambo.

Hakika Uislamu ndio dini inayokwenda sambamba na akili salama na maumbile ya sawa, kwani inatoa majibu ya kimantiki ya maswala ya uwepo mkuu: Kwa nini sisi tuko hapa? Na ni lipi lengo la maisha yetu? Na yapi mafikio baada ya kifo?

Na Uislamu unasimama katika msingi wa kumpwekesha Muumba katika ibada, na kushuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, hii ndio shahada ya kwanza, na ndio msingi na asili ya imani katika Uislamu, na inakusudia kuwa hakuna muabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake.

Na shahada hii inajumuisha yafuatayo:

Tauhidi: Yaani kumuamini mola anayestahiki ibada peke yake asiyekuwa na mshirika, wala hana mtoto, wala wa kufanana naye.

Kujitenga mbali na ushirikina: Yaani kuyakemea masanamu yote na miungu ya kutengenezwa na watu.

Na Uislamu unawajibisha kuwaamini Mitume wote. Waislamu wanawaamini - kama

alivyoeleza Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani - ya kuwa Issa (Yesu) ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kwamba yeye si mwana wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu, Mwenyezi Mungu ni Mtukufu na haimuwezekanii kuwa na mke au mtoto. Yeye amejitosheleza na hawahitaji wao wala hahitaji kitu chochote kile. Mwenyezi Mungu ametueleza ndani ya Qur'ani ya kuwa Issa alikuwa Nabii, Mwenyezi Mungu alimpa miujiza mingi, na kwamba Mwenyezi Mungu alimtuma kuwaita watu wake ili kumuabudu peke yake asiye na mshirika, na akatueleza kuwa Issa hakuwataka watu wamuabudu yeye, bali hata yeye mwenyewe alikuwa akimuabudu Muumba wake. Hivyo basi, ukitaka kuwa Muumini wa Issa (Yesu) kwa imani ya kweli anayoipenda Mwenyezi Mungu, basi unatakiwa kuingia ndani ya Uislamu.

Na ametueleza Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani kuwa Issa aliwaamrisha watu wake kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na akawatahadharisha na ushirikina.

Hivi ni mantiki na inaingia akilini kwa

mwenye akili kumuabudu kiumbe mfano wake, anayepata njaa na kiu na wala hamiliki kujizuilia na kifo au madhara?! Sasa wewe mwanadamu unamuabudu vipi Yesu mwana wa Mariam hali yakuwa ni mwanadamu aliyekuwa akihitaji chakula na kinywaji, na alikuwa akimuelekea muumba wake kwa sala?! Hivi inawezekana kwa mwenye akili kuvuta picha kuwa eti mungu anasali?! Kwani Mwenyezi Mungu si ndiye anayesifika kwa utukufu, aliyepwekeka katika ukamilifu wake, aliyeepukana na kushabihiana na kufanana, na kila kilichoko ulimwenguni kiko chini ya uwezo wake na mamlaka yake? Inawezekana vipi kujishusha hadhi muumba wa mbingu na Ardhi azaliwe kama mtoto, kisha ajisalimishe kwa viumbe wake ili wamsulubu? Bila shaka wanaosulubiwa na kuuawa ni binadamu wanaomalizika. Ama Muumbaji, yeye yu hai na hafi, Msimamizi wa mambo yote, asiyeshikwa na usingizi wala kulala. Basi je, si katika ukamilifu wa utukufu wake atakaswe mbali wa mambo mfano wa hayo?

Bila shaka alitueleza Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani tukufu kuwa Mitume wote walikuja

na ujumbe mmoja ambao muhutasari wake ni kuwalingania watu wao kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika. Lakini baada ya kupita zama nyingi, baadhi yao walipotosha ujumbe huu wa milele, wakaifuta nuru ya suala la kumpwekesha Mwenyezi Mungu walilokuja nalo Manabii. Basi Mwenyezi Mungu akamtuma wa mwisho katika Mitume, Muhammadi - rehema na amani ziwe juu yake - na akamteremshia Qur'ani tukufu ili aurudishe upya ujumbe wa kumpwekesha Mwenyezi Mungu waliokuja nao Mitume wote kabla yake.

## Na kwa kuhitimisha tunakuambia ewe mwanadamu:

Hakika Uislamu ndiyo dini ya akili na maumbile yaliyo salama, na ndiyo dini ya pekee aliyoiweka Muumba Mtukufu kuwa sheria kwa wanadamu. Basi ni wajibu kwa kila mwanadamu mwenye akili timamu afanye haraka kuingia ndani ya Uislamu, na hilo ni kwa kumuamini Mwenyezi Mungu kuwa ndiye Mola Mlezi, na Uislamu kuwa ndio dini, na Muhammadi kuwa ndiye Mtume, na jambo hili

mwanadamu hana hiyari ndani yake. Kwa sababu Mwenyezi Mungu atamuuliza Siku ya Kiyama juu ya kile alichowajibu Mitume. Endapo atakuwa Muumini, basi atafuzu na atafaulu kufaulu kukubwa. Na akiwa kafiri, basi atakuwa na hasara ya wazi.

Ikiwa unatafuta furaha ya kweli katika dunia na kufaulu Akhera, basi tambua kuwa maamuzi makubwa zaidi unayoweza kuyachukua katika maisha yako ni kuingia ndani ya Uislamu. Na hakuna la wajibu juu yako zaidi ya kutamka maneno haya kutoka ndani ya moyo kwa imani ya kweli: "Ash-hadu an laa ilaaha illallah, wa ash-hadu anna Muhammadan rasuulullah (Ninashuhudia kuwa hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninashuhudia kwamba Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu)", kisha anza kujifunza dini yako na kuyafanyia kazi yale yanayotakiwa na shahada mbili hizi ikiwemo kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kushikamana na nguzo za Uislamu.

Yaseme sasa hivi, na wala usisitesite. Kwani kifo kinaweza kuja ghafla, usicheleweshe

maamuzi yenye umuhimu mkubwa kama haya. Usimuachie Shetani fursa ya kukuzuilia mbali na kheri. Kuwa shujaa na anza njia yako leo ya kuelekea katika nuru na uongofu.

Fanya maamuzi sasa hivi, na anza maisha mapya yaliyojaa utulivu na radhi.

"Ash-hadu an laa ilaaha illallah, wa ash-hadu anna Muhammadan rasuulullah (Ninashuhudia kuwa hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu)."

❊❊❊

جمعية خدمة المحتوى
الإسلامي باللغات

Kitabu hiki kinahusu swali la uwepo na uumbaji, na kinathibitisha kwa akili uwepo wa muumbaji mwenye hekima kamilifu na Mkamilifu. Vile vile, kinaweka wazi kwamba lengo kuu la maisha ni kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na kwamba Uislamu ndio Dini ya kweli iliyohifadhiwa. Inawaita watu kumuamini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Muhammadi na kufuata mafundisho yake, na inatahadharisha dhidi ya ushirikina. Vile vile, inatilia mkazo suala la kuulizwa juu ya matendo na kulipwa huko Akhera.